

UMUHIMU WA UMOJA WA KITAIFA

Umoja ni hali ya kufanya mambo kwa ushirikiano bila kujitenga. Mambo mengi huweza kufanyika vizuri iwapo kuna ushirikiano baina ya wahusika. Kujaribu kujifanyia mambo bila kusaidiana na wengine si jambo zuri. Je, umoja wa kitaifa una umuhimu upi? Jambo la kwanza, umoja wa kitaifa huleta ushirikiano baina ya wananchi. Ushirikiano huu huwa katika nyanja mbalimbali kama vile kazini, katika biashara na michezoni. Watu wanaposhirikiana katika shughuli zao, bila shaka wao hufaulu.

Aidha, umoja huimarisha amani katika nchi yetu. Amani ni muhimu sana katika nchi. Vita na chuki ni adui sana kwa taifa hili. Nchi yenye amani hupiga hatua mno katika kila sehemu. Vita huharibu mali na maisha ya watu. Watu wengi huaga dunia wakati wa vita. Mali pia huharibiwa wakati wa vita. Kwa hivyo, ni vyema kuhakikisha kuwa tunaishi kwa amani na umoja. Pakitokea kosa lolote kati yetu, ni vizuri kuzungumza na kuelewana. Kusameheana ni jambo muhimu sana. Unapokosewa na mtu yeyote, kumbuka kuwa wewe pia hukosea. Wakenya tupendane na kuishi kwa amani.

Kadhalika, umoja huiwezesha serikali kushughulikia mambo muhimu ya taifa. Badala ya kutumia rasilimali za nchi katika kukabiliana na uhalifu, serikali hutumia muda wake kulijenga taifa. Katika nchi ambayo haina umoja, serikali hutumia wakati mwingi kuwatuliza wananchi na kuwaeleza kuhusu umuhimu wa kuwa na ushirikiano. Katika hali hiyo, maendeleo hurudi chini. Tunapoishi kwa amani, serikali yetu hutumia pesa na wakati wake kushughulikia mambo mengine.

Umoja wa kitaifa huchangia mno katika maendeleo ya kitaifa. Katika nchi yenye umoja, wananchi hushirikiana katika shughuli zao. Kwa hivyo, ni rahisi sana kufaulu katika kila walifanyalo. Kufaulu katika kazi na biashara huwapa wananchi pesa. Pesa hizo hutumika kuanzishia miradi mingine ya maendeleo. Vilevile, ushuru ambao hulipwa na wafanyakazi na wafanyabiashara hutumiwa na serikali katika ujenzi wa barabara, hospitali na kadhalika.